ISSN 0856-6976

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

## *Mapitio ya Nusu Mwaka 2020/21*

**GAVANA**

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**Februari 2021**

ISSN 0856-6976

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

## *Mapitio ya Nusu Mwaka*

## *2020/21*

**GAVANA**

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**Februari 2021**

## Utangulizi

Tamko la Sera ya Fedha ambalo lilitolewa mwezi Juni 2020 lilieleza kwa kina malengo na mikakati ya Benki Kuu ya Tanzania ya utekelezaji wa sera ya fedha kwa mwaka 2020/21, ili kuwezesha mfumuko wa bei kuwa mdogo na tulivu, na kusaidia ukuaji wa uchumi. Katika taarifa hii ya mapitio ya kipindi cha nusu ya mwaka ya Tamko la Sera ya Fedha, Benki Kuu ya Tanzania inatoa tathmini ya mwenendo wa uchumi wa Tanzania na wa dunia kwa mwaka 2020. Aidha, taarifa hii inatoa tathmini ya utekelezaji wa malengo na mikakati iliyoainishwa katika Tamko la Sera ya Fedha la mwezi Juni 2020. Vilevile, taarifa hii inatoa mwelekeo wa uchumi wa Tanzania na wa dunia, pamoja na mwelekeo wa sera ya fedha katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2020/21 ili kuwezesha kuendelea kuwa na mfumuko mdogo wa bei na kusaidia ukuaji wa uchumi.

## Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Uchumi wa dunia umeimarika kidogo katika siku za hivi karibuni, licha ya changamoto ya kuibuka tena maambukizi ya ugonjwa wa Corona (COVID-19) katika nchi kadhaa. Ripoti ya Jumuiya ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD)[1] ya mwezi Desemba 2020 inaonyesha uchumi wa nchi nyingi duniani kuimarika katika robo ya tatu ya mwaka 2020, tofauti na robo ya pili ya mwaka 2020 ambapo uchumi ulidorora. Hata hivyo, licha ya ukuaji kuanza kuimarika, taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya mwezi Januari 2021 inakadiria uchumi wa dunia kushuka kwa asilimia

1 The Organisation for Economic Co-operation and Development (OECD)

3.5 katika mwaka 2020, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.8 mwaka 2019. Kushuka huku kwa uchumi kunatokana na hatua zilizochukuliwa na nchi mbalimbali kudhibiti ugonjwa wa Corona, ambazo ziliathiri shughuli za biashara, uwekezaji na uzalishaji duniani. Hatua hizo ni pamoja na kuzuia watu kutoka nje ya makazi yao (lockdown) na zuio la safari za kimataifa ili kuzuia maambukizi ya janga hilo. Uchumi wa nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara unakadiriwa kushuka kwa asilimia 2.6 mwaka 2020, hususan katika nchi zinazotegemea zaidi uzalishaji na uuzaji wa mafuta nje ya nchi kutokana na bei ya mafuta kushuka katika soko la dunia.

IMF inakadiria kuwa uchumi wa dunia utaimarika na kuweza kukua kwa asilimia 5.5 mwaka 2021, kutokana na kuendelea kupungua kwa ugonjwa wa Corona katika nchi nyingi duniani. Hali hii inatokana na hatua zinazochukuliwa kudhibiti maambukizi ya Corona katika nchi nyingi duniani. Kupungua kwa ugonjwa wa Corona kutawezesha kulegezwa kwa hatua zilizochukuliwa kudhibiti kusambaa kwa ugonjwa huo. Katika nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara, ukuaji wa uchumi unakadiriwa kuwa asilimia 3.2 mwaka 2021, kutokana na kuimarika kwa sekta mbalimbali ikiwemo biashara na utalii, ambayo iliathirika sana kutokana na janga la Corona. Hata hivyo, kuibuka kwa maambukizi mapya ya ugonjwa huo katika baadhi ya nchi hivi karibuni kunaweza kuathiri ukuaji wa uchumi wa dunia. Hii inatokana na baadhi ya nchi kurejesha njia za awali za kuzuia kusambaa kwa ugonjwa huo, ikiwemo kufunga mipaka na kusimamisha baadhi ya shughuli za kiuchumi. Vilevile, ripoti ya Benki ya Dunia iliyotolewa mwezi Januari 2021 inakadiria

kuwa uchumi wa dunia utashuka kwa asilimia 4.3 mwaka 2020, na kukua kwa asilimia 4.0 mwaka 2021. Aidha, ripoti hiyo inaonyesha kuwa ukuaji wa uchumi wa nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara unakadiriwa kupungua kwa asilimia 3.7 mwaka 2020 na kukua kwa asilimia 2.7 mwaka 2021.

Mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea na nchi zinazoibukia kiuchumi umeendelea kubaki katika viwango vya chini kutokana na athari za janga la Corona. Kuanzia mwezi Julai hadi Desemba 2020 mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea ulishuka kutokana na kupungua kwa bei ya nishati, wakati katika nchi zinazoibukia kiuchumi mfumuko wa bei ulishuka kutokana na kupungua kwa bei ya chakula. Wastani wa mfumuko wa bei kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ulikuwa asilimia 5.2, kiwango ambacho ni chini ya kiwango cha juu cha asilimia 8.0 kwa mujibu wa vigezo vya mtangamano wa kiuchumi wa Jumuiya. Pia katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), viwango vya mfumuko wa bei vilibaki ndani ya wigo wa kati ya asilimia 3-7.0 uliowekwa kwa mujibu wa vigezo vya mtangamano wa kiuchumi wa Jumuiya, isipokuwa katika nchi za Angola, Zambia na Zimbabwe. Katika mwaka 2021, mfumuko wa bei unakadiriwa kubaki katika viwango vya chini katika nchi nyingi duniani, na kuongezeka kidogo kutokana na kuimarika kwa mahitaji na ongezeko la bei za nishati. Katika nchi zilizoendelea na nchi zinazoibukia kiuchumi, mfumuko wa bei unatarajiwa kufikia asilimia 1.3 na asilimia 4.2 mwaka 2021, kwa mpangilio huo. Mfumuko wa bei unatarajiwa kupungua katika nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara hadi kufikia asilimia 7.9

mwaka 2021, kutoka asilimia 10.6 iliyokadiriwa mwaka 2020. Hali hii inatokana na matarajio ya utulivu wa bei za chakula, iwapo hazitatokea athari katika uzalishaji na mfumo wa kibiashara.

## Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

### *Tanzania Bara*

Uchumi umeendelea kuwa imara licha ya athari za janga la COVID-19 katika uchumi wa dunia zilizosababisha baadhi ya shughuli za kiuchumi nchini kuathirika. Pato la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 4.7 katika miezi tisa ya kwanza ya mwaka 2020, ikilinganishwa na asilimia 7.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2019 na asilimia 6.9 kwa mwaka 2018. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na shughuli za ujenzi, kilimo, uchukuzi na uchimbaji madini. Aidha, ukuaji huo ulitokana na uwekezaji ambao Serikali inafanya katika miundombinu, ukichangiwa na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi na sera madhubuti ya bajeti ya Serikali. Kasi ya kuridhisha ya ukuaji wa uchumi ilitokana pia na uamuzi wa Serikali wa kutofunga shughuli za kiuchumi kufuatia mlipuko wa COVID-19, isipokuwa kufunga kwa muda shule, shughuli za michezo na burudani na kusimamisha safari za ndege za abiria kuanzia mwezi Machi hadi Juni 2020. Ukuaji wa uchumi unakadiriwa kuwa asilimia 5.5 mwaka 2020 na asilimia 6.0 au zaidi katika mwaka 2021 kutokana na utekelezaji wa mipango ya maendeleo, kuimarika kwa uchumi wa dunia na uwekezaji wa sekta binafsi.

Mfumuko wa bei umeendelea kuwa tulivu katika kiwango cha chini, ambapo ulifikia wastani wa asilimia 3.2 katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2020, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Katika kipindi chote, mfumuko wa bei ulikuwa ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 5.0 na ndani ya wigo uliowekwa kwa mujibu wa vigezo vya mtangamano wa kiuchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kiwango ambacho hakizidi asilimia 8.0. Pia, kiwango cha mfumuko wa bei kilibaki ndani ya wigo uliowekwa na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wa kati ya asilimia 3.0 na 7.0. Kiwango hicho cha mfumuko wa bei kilitokana na upatikanaji wa chakula cha kutosha, bei ndogo ya mafuta kwenye soko la dunia, utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani na sarafu nyingine duniani, na sera madhubuti ya fedha na sera ya bajeti. Utulivu na kiwango kidogo cha mfumuko wa bei katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2020/21 unatarajiwa kuendelea katika kipindi kilichobaki cha mwaka wa fedha, kutokana na matarajio ya hali nzuri ya hewa na upatikanaji wa chakula cha kutosha, bei ndogo ya mafuta katika soko la dunia, na utulivu wa kiwango cha kubadilisha shilingi dhidi ya fedha za kigeni. Hata hivyo, hali ya upungufu wa chakula katika baadhi ya nchi jirani, iliyosababishwa na nchi hizo kufunga baadhi ya shughuli za kiuchumi kufuatia mlipuko wa COVID-19, inaweza kusababisha mfumuko wa bei kuongezeka kwa kiasi.

Ujazi wa fedha umeendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha kutokana na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi katika uchumi, licha ya changamoto zilizotokana na athari za COVID-19. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 7.1 katika kipindi kinachoanzia mwezi Julai hadi mwezi Desemba 2020, ikilinganishwa na asilimia 9.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Kiwango cha ukuaji wa M3 kilikuwa ndani ya wigo uliowekwa, yaani ukuaji usiozidi asilimia 10.0 kwa mwaka utakaoishia mwezi Juni 2021. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) uliongezeka kwa wastani wa asilimia 9.6, ikilinganishwa na asilimia 11.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Vilevile, wastani wa ukuaji wa fedha taslimu ulikuwa asilimia 3.3, ikilinganishwa na asilimia 8.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2019, na lengo la wastani wa ukuaji wa asilimia 9.5 ifikapo mwisho wa mwezi Juni 2021. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa M3 kuliendana na kuongezeka kwa kasi ya mzunguko wa fedha kufuatia ongezeko la kufanya malipo kwa njia ya kidigitali. Kasi ya kukua kwa ujazi wa fedha inatarajiwa kuongezeka hadi wastani wa asilimia 10.0 ifikapo mwishoni mwa mwezi Juni 2021 kama ilivyokadiriwa hapo awali, sambamba na ongezeko la mzunguko wa fedha, kutokana na shughuli za biashara na uwekezaji nchini kuendelea kuimarika.

Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulikuwa wa wastani wa asilimia 5.1 katika kipindi cha mwezi Julai hadi mwezi Desemba 2020, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 9.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Kasi ndogo ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ilitokana na athari hasi za COVID-19 kwenye uchumi wa

dunia, ambao uliathiri baadhi ya biashara nchini, hususan shughuli zinazohusiana na utalii na usafirishaji, na hivyo kusababisha mahitaji ya mikopo mipya kupungua. Sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi ilielekezwa kwenye shughuli binafsi (biashara ndogondogo na biashara za kati), uchukuzi na mawasiliano, na madini. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi unatarajiwa kuimarika katika kipindi kilichobaki cha mwaka wa fedha 2020/21, kutokana na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi, sera madhubuti ya bajeti, kurejea kwa shughuli za kiuchumi na kufunguka kwa uchumi wa dunia, pamoja na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali na Benki Kuu ya Tanzania katika kuboresha mazingira ya biashara, kupunguza riba za mikopo, na mabenki kuongeza mikopo kwa sekta binafsi.

Shilingi ya Tanzania imeendelea kuwa imara dhidi ya fedha za kigeni katika kipindi cha mwezi Julai hadi mwezi Desemba 2020. Katika soko la jumla la fedha za kigeni, dola moja ya Marekani ilikuwa ikibadilishwa kwa kati ya shilingi 2,304.23 na shilingi 2,309.97, ikilinganishwa na wigo wa kati ya shilingi 2,299.26 na shilingi 2,300.95 kwa dola ya Marekani katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Viwango hivi ni sawa na kupungua kwa thamani ya shilingi kwa wastani wa asilimia 0.4 katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba 2020, ikilinganishwa na kupungua kwa asilimia 0.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Kiwango hiki kidogo cha kupungua kwa thamani ya shilingi kimetokana na mfumuko mdogo wa bei, utekelezaji wa sera thabiti za fedha na bajeti, bei ndogo ya mafuta katika soko la dunia na nakisi ndogo ya urari wa biashara

ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nchi za nje. Aidha, hatua zilizochukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania katika kuhakikisha uwazi na utulivu katika shughuli za soko la fedha za kigeni zimechangia katika kuimarisha utulivu wa shilingi. Thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani inatarajiwa kuendelea kuwa imara katika kipindi kilichobaki cha mwaka wa fedha 2020/21 kutokana na mfumuko mdogo wa bei, sera thabiti za fedha na bajeti, na utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni na bei ya mafuta katika soko la dunia.

Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2020, utekelezaji wa sera ya bajeti ulikuwa wa kuridhisha. Ukusanyaji wa mapato ya ndani ulikuwa kiasi cha shilingi bilioni 10,467.2, sawa na asilimia 89.0 ya lengo. Kwa mwezi Desemba 2020, mapato ya ndani yalikuwa juu ya lengo kutokana na jitihada nzuri za ukusanyaji zilizofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania, ambapo mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 2,046.8, juu ya lengo la shilingi bilioni 1,977.1. Mafanikio haya yanatokana na mwenendo mzuri wa ukuaji wa uchumi na jitihada za Serikali za kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji mapato, ikiwemo matumizi ya teknolojia. Matumizi ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 10,856.5, ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 6,932.6 na matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 3,923.9.

Deni la ndani na nje la Serikali limeendelea kuwa himilivu, na thamani yake kwa sasa ni asilimia 27.9 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 70. Hali hii imechangiwa na matarajio mazuri

ya ukuaji wa uchumi, pamoja na utekelezaji wa sera thabiti katika kusimamia uchumi wa nchi. Hadi mwishoni mwa mwezi Desemba 2020, deni la Serikali lilifikia dola za Marekani milioni 25,583.8 kutoka dola milioni 24,553.3 mwishoni mwa mwezi Juni 2020, ambapo deni la nje likiwa ni asilimia 72.5.

Sekta ya nje imeendelea kuwa na matokeo mazuri, licha ya changamoto zinazotokana na janga la COVID-19 kwenye shughuli mbalimbali za kibiashara, utalii na uwekezaji. Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nchi za nje imepungua kutokana na ongezeko la mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, na kupungua kwa uagizaji bidhaa na huduma kutoka nchi za nje. Nakisi hiyo inakadiriwa kubaki katika viwango vya chini, wastani wa asilimia 3.6 ya Pato la Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/21. Hata hivyo, kuibuka tena kwa maambukizi mapya ya COVID-19 kunaweza kuwa na athari katika mauzo ya nje ya nchi, hususan utalii, hoteli na malazi. Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yalifikia dola za Marekani milioni 4,601.4 katika kipindi cha mwezi Julai hadi mwezi Desemba 2020, mauzo makubwa zaidi yakiwa ni ya dhahabu, bidhaa za bustani, na bidhaa za viwandani. Uagizaji bidhaa na huduma ulifikia dola za Marekani milioni 4,565.8, zikijumuisha zaidi uagizaji wa mashine, vifaa vya ujenzi, vyombo vya usafirishaji, malighafi za viwandani na mafuta. Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kubaki katika viwango vya kuridhisha na kufikia jumla ya dola za Marekani milioni 4,767.7 mwishoni mwa mwezi Desemba 2020. Akiba hii inatosha kulipia uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa takriban miezi 5.6, kiwango

ambacho ni ndani ya lengo la nchi la kuwa na akiba isiyopungua miezi minne.

Sekta ya benki imeendelea kuwa imara, stahimilivu, yenye mtaji wa kutosha, faida ya kutosha na kiwango cha kuridhisha cha ukwasi. Ubora wa rasilimali za mabenki uliimarika kutokana na kupungua kwa uwiano wa mikopo chechefu kwenye mikopo yote na kufikia asilimia 9.3 mwezi Desemba 2020 kutoka asilimia 10.8 kwa mwezi Juni 2020. Aidha, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kuimarisha usimamizi wa sekta ya fedha kwa kutekeleza sera na kutoa miongozo mbalimbali ili kulinda uimara wa sekta hiyo. Vilevile, mabenki yalielekezwa kutekeleza mipango ya kuwa na mitaji juu ya kiwango kinachotakiwa kisheria ili kuongeza mikopo kwa sekta binafsi na huduma zingine za benki. Sekta ya benki inatarajiwa kubaki salama na tulivu, sambamba na sera zinazotekelezwa na hatua zinazochukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania katika kuboresha mazingira ya biashara na ufanisi katika utoaji wa huduma za fedha. Vilevile, Benki Kuu ya Tanzania inaendelea kufuatilia ubora wa rasilimali za sekta ya benki kwa lengo la kupunguza mikopo chechefu hadi kufikia kiwango kinachotarajiwa na Benki Kuu ya Tanzania, kisichozidi asilimia 5.

Mifumo ya malipo imeendelea kufanya kazi kwa ufanisi, ikiwa ni pamoja na ongezeko la matumizi ya njia za kidigitali katika utoaji wa huduma za fedha nchini. Benki Kuu ya Tanzania imetekeleza mfumo wa usajili wa watoa huduma za fedha ili kuonyesha maeneo vilipo vituo vya kutolea huduma za fedha kote nchini. Hatua hii

itawezesha watunga sera kufanya tathmini kwa urahisi zaidi juu ya maeneo muhimu kwa ajili ya utoaji wa huduma za fedha. Pia, mfumo huu utasaidia wasimamizi na wawekezaji katika sekta ya fedha kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi zaidi. Mfumo huu pia utaboresha huduma jumuishi za fedha kwa kuwezesha watumiaji wa huduma kujua mahali vituo vilipo, na hivyo kufanya uamuzi sahihi. Aidha, Benki Kuu ya Tanzania inaendelea kutengeneza mfumo wa malipo ya papo kwa papo wa Tanzania, ambao utaunganisha mifumo mbalimbali ya malipo nchini. Kwa kuunganisha mifumo mbalimbali ya malipo kupitia mfumo huo gharama za malipo zitapungua, usimamizi wa watoa huduma utaimarika na huduma jumuishi za fedha zitapanuka.

***Zanzibar***

Uchumi wa Zanzibar ulikua kwa wastani wa asilimia 1.5 katika kipindi cha robo tatu za mwaka 2020, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Sababu mojawapo ya kiwango hiki kidogo cha ukuaji ni kudorora kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi kama vile malazi na huduma za chakula, uchukuzi na uhifadhi mizigo, na habari na mawasiliano, ambazo ziliathiriwa kwa kiwango kikubwa na janga la COVID-19. Kasi ya ukuaji wa uchumi inatarajiwa kuongezeka katika nusu ya pili ya mwaka 2020/21 na baadae, kutokana na matarajio ya kuendelea kufunguka kwa shughuli za kiuchumi duniani, hali itakayosababisha kuimarika kwa shughuli za kiuchumi, hususan katika sekta ya utalii. Aidha, utekelezaji wa mipango ya maendeleo ikiwemo kuongeza wigo wa shughuli za kiuchumi, utachangia kasi ya ukuaji wa uchumi.

Mfumuko wa bei umeendelea kuwa mdogo na tulivu, ambapo ulifikia wastani wa asilimia 1.9 katika kipindi cha mwezi Julai hadi mwezi Desemba 2020, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Kiwango hiki cha mfumuko wa bei kilitokana na kupungua kwa bei za bidhaa zisizo za chakula, hususan mafuta ya petroli na dizeli. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kuwa mdogo na tulivu katika nusu ya pili ya mwaka wa fedha 2020/21, kutokana na kuimarika kwa shughuli za uzalishaji na biashara baada ya baadhi ya nchi kuanza kupunguza vikwazo vilivyowekwa kwa ajili ya kukabiliana na janga la mlipuko wa COVID-19.

Ukusanyaji wa mapato ya ndani ulikuwa shilingi bilioni 302.5 katika kipindi cha mwezi Julai hadi mwezi Desemba 2020, sawa na asilimia 59.9 ya lengo. Matokeo haya yametokana na athari za janga la COVID-19 kwenye vyanzo vikuu vya mapato, hususan utalii. Mapato yatokanayo na kodi yalifikia asilimia 57.5 ya lengo, wakati mapato yasiyo ya kodi yalifikia asilimia 86.8 ya lengo. Ukusanyaji wa mapato unatarajiwa kuongezeka katika nusu ya pili ya mwaka 2020/21 kutokana na kuanza kuimarika kwa shughuli zinazohusiana na utalii, pamoja na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Katika kipindi hicho, jumla ya matumizi yalifikia shilingi bilioni 472.3, sawa na asilimia 83.3 ya makadirio, matumizi ya kawaida yakiwa shilingi bilioni 353.2 na matumizi ya maendeleo yakiwa shilingi bilioni 119.1. Deni la Serikali liliongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 896.6 mwishoni mwa mwezi Desemba 2020, kutoka shilingi bilioni 824.5 mwishoni mwa mwezi Juni 2020, ambapo deni la nje likiwa asilimia 77.1.

Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nchi za nje katika kipindi cha mwezi Julai hadi mwezi Desemba 2020 iliongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 107.9, ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 46.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Mwenendo huu ulitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa na huduma, pamoja na kupungua kwa mapato yatokanayo na huduma za kitalii. Uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi uliongezeka kwa asilimia 18.7 hadi dola za Marekani milioni 252.9, wakati mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi ulipungua kwa asilimia 28.3 hadi dola za Marekani milioni 92.3.

## Utekelezaji wa Malengo ya Sera ya Fedha Katika Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2020/21

Malengo ya sera ya fedha kwa mwaka wa fedha 2020/21 yaliwekwa kwa kuzingatia madhara ya janga la COVID-19 kwa uchumi wa dunia na athari zake katika uchumi wa Tanzania. Utekelezaji wa sera ya fedha ulikusudia kufikia lengo la ukuaji wa Pato la Taifa la asilimia 5.5 kwa mwaka 2020, na kuhakikisha kuwa mfumuko wa bei unabaki ndani ya wigo wa kati ya asilimia 3.0 na asilimia 5.0. Ili kutimiza malengo haya, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kutekeleza sera ya fedha yenye malengo yafuatayo:

i. ukuaji wa fedha taslim wa asilimia 9.5;
ii. ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 10.0;
iii. ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 11.6; na
iv. kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Katika kipindi cha mwezi Julai hadi mwezi Desemba 2020, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la kuongeza ukwasi kwenye uchumi, hatua iliyochangiwa na kuwepo kwa mfumuko mdogo wa bei. Utekelezaji wa sera ya fedha ulilenga kufufua shughuli mbalimbali za uchumi zilizokuwa zimeathiriwa na madhara ya janga la COVID-19 kwa kuwezesha sekta ya benki kutoa mikopo kwa gharama nafuu kwa sekta binafsi. Ili kufikia lengo hilo, Benki Kuu ya Tanzania iliongeza ukwasi katika sekta ya benki kwa kutumia nyenzo mbalimbali, hususan kwa kutoa mikopo ya muda mfupi kwa mabenki na kununua fedha za kigeni kutoka kwenye soko la ndani la fedha za kigeni.

Utekelezaji wa sera ya fedha ulisaidia kuimarika kwa ukwasi katika sekta ya benki, hivyo kusababisha riba katika masoko ya fedha kupungua. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2020/21, riba ya siku moja katika soko la fedha baina ya mabenki ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 3.50 kutoka asilimia 4.57 katika kipindi kama hicho mwaka 2019 na asilimia 4.27 katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi mwezi Juni 2020. Vilevile, riba ya jumla ya dhamana za Serikali za muda mfupi ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 4.00 kutoka asilimia 6.84 kwa kipindi cha mwezi Julai hadi mwezi Desemba 2019 na asilimia 4.85 katika kipindi cha mwezi Januari hadi mwezi Juni 2020. Aidha, wastani wa viwango vya riba za mikopo ya mabenki ulipungua, japo kwa kasi ndogo, hadi kufikia asilimia 16.57 katika kipindi cha mwezi Julai hadi mwezi Desemba 2020 kutoka wastani wa asilimia 16.85 katika kipindi cha mwezi Julai hadi mwezi Desemba 2019. Wakati

huo huo, wastani wa riba za amana kwa ujumla ulikuwa asilimia 6.60 kutoka asilimia 7.15.

Sambamba na utekelezaji wa sera wezeshi ya fedha iliyolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi, ujazi wa fedha na mikopo kwa sekta binafsi umeendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha. Katika kipindi cha mwezi Julai 2020 hadi mwezi Desemba 2020, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi, M3, ulikua kwa wastani wa asilimia 7.1, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 9.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulifikia wastani wa asilimia 5.1, ikilinganishwa na asilimia 9.3 katika kipindi cha mwezi Julai hadi mwezi Desemba 2019. Mwenendo huu wa ukuaji wa ujazi wa fedha na mikopo kwa sekta binafsi ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kudorora kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi kufuatia changamoto zilizosababishwa na janga la COVID-19. Hata hivyo, kuongezeka kwa kasi ya mzunguko wa fedha sambamba na ongezeko la matumizi ya huduma za fedha za kidigitali kulisaidia kupunguza athari za ukuaji mdogo wa ujazi wa fedha kwenye shughuli mbalimbali za kiuchumi.

**Mwelekeo wa Uchumi**

Uchumi wa Tanzania unatarajiwa kuendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka wa fedha 2020/21 na baadae. Ukuaji wa uchumi utachangiwa zaidi na uwekezaji kwenye miundombinu, hali nzuri ya hewa kwa kilimo, na utekelezaji endelevu wa sera madhubuti ya fedha na sera ya bajeti.

Hata hivyo, kasi ya ukuaji wa uchumi itaongezeka kadiri shughuli za kibiashara na uwekezaji katika soko la dunia zinavyoimarishwa, pamoja na uboreshaji mazingira ya kufanya biashara nchini. Katika mwaka 2021, uchumi unakadiriwa kukua kwa asilimia 6[2] au zaidi kutokana na utekelezaji wa mipango ya maendeleo na kuimarika kwa uchumi wa dunia.

Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kuwa mdogo na tulivu, kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0, katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka wa fedha 2020/21. Matarajio haya yanachangiwa zaidi na hali nzuri ya hewa kwa kilimo cha chakula, utulivu katika bei ya mafuta katika soko la dunia na utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni. Aidha, utekelezaji wa sera thabiti ya fedha na sera ya bajeti ya Serikali utaendelea kuweka mazingira mazuri ya kudumisha utulivu wa mfumuko wa bei katika viwango vya chini.

## Mwelekeo wa Sera ya Fedha Katika Kipindi cha Nusu ya Pili ya Mwaka 2020/21

Katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka wa fedha 2020/21, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la kuongeza ukwasi katika uchumi. Msukumo wa kuongeza ukwasi katika uchumi unatokana na matarajio ya kuongezeka kwa ukuaji wa uchumi, kiwango kidogo na tulivu cha mfumuko wa bei, na lengo la kuchochea ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Utekelezaji huu unalenga kuhakikisha kuwa mikopo kwa sekta binafsi na ujazi wa fedha unakua kwa kasi iliyotarajiwa, kuongeza ufanisi katika kutoa huduma za kifedha, na kusaidia kupungua kwa riba za mikopo.

2 Maoteo ya awali yaliyofanyika mwaka 2020.

Kutokana na matarajio hayo, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kutumia nyenzo mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha hali ya ukwasi inaendelea kubaki katika viwango vya kukidhi mahitaji ya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Vilevile, katika kutekeleza majukumu yake, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kuboresha masoko ya fedha pamoja na kuweka miundombinu wezeshi, kutoa miongozo na elimu kwa umma ili kuongeza tija.

**Hitimisho**

Ukuaji wa uchumi wa nchi yetu unatarajiwa kuendelea kuimarika katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka wa fedha 2020/21 na baadae, kutokana na kuendelea kutekeleza sera wezeshi za kiuchumi, pamoja na hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kusimamia rasilimali za taifa. Uboreshaji wa mazingira ya kibiashara na kuendelea kufunguka kwa uchumi wa dunia ni baadhi ya mambo muhimu yanayotarajiwa kuchangia katika ukuaji wa uchumi wetu. Kasi ya ukuaji wa uchumi itapata pia msukumo zaidi kutokana na uwekezaji unaofanywa na Serikali na sekta binafsi, upatikanaji wa nishati ya uhakika, utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi na matarajio ya hali nzuri ya hewa. Hivyo, lengo la ukuaji wa uchumi la asilimia 5.5 mwaka 2020 na asilimia 6 mwaka 2021 yatafikiwa. Aidha, ukuaji wa uchumi unatarajiwa kuwa mkubwa zaidi katika mwaka 2021 kwa kuzingatia kuanza tena kwa shughuli za kiuchumi katika soko la dunia ambazo ziliathirika zaidi na janga la COVID-19. Kuongezeka kwa shughuli za uchumi wa ndani kutasaidia pia ongezeko la ukusanyaji wa mapato ya kodi

na kuchangia sera ya bajeti kutoa mchango mkubwa zaidi katika kuimarisha uchumi wa nchi. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya lengo la kati ya asilimia 3.0 na asilimia 5.0 katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka wa fedha 2020/21.

Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la kuongeza ukwasi katika uchumi kutokana na mfumuko wa bei kuendelea kuwa mdogo na tulivu. Utekelezaji huu utaambatana na hatua thabiti za kusimamia sekta ya fedha ili kuboresha upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa wawekezaji na wafanyabiashara, kudumisha mazingira wezeshi ya kiuchumi na kuimarisha sekta ya fedha kwa ajili ya kuongeza mchango wa sekta binafsi katika ukuaji wa uchumi. Ni matarajio ya Benki Kuu ya Tanzania kuwa malengo ya sera ya fedha yaliyowekwa katika Tamko la Sera ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2020/21 yatafikiwa.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi
Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, 11884 Dar es Salaam
Simu: +255 22 2233328/9, Nukushi: +255 22 2234060
Tovuti: http://www.bot.go.tz